# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA HAMSINI NA SABA

**25 JUNI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA HAMSINI NA SABA – TAREHE 25 JUNI, 2026

**I. DUA:**

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**678. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (MISSENYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga Shule za Sekondari katika Kata za Mutukula, Kyaka na Bugohora Wilayani Missenyi.

**679. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Ipazya Isalalo katika Mto Nkana Kata ya Ipunga.

**680. MHESHIMIWA DKT. NEEMA PETER MAJULE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vikundi vinavyopata Mikopo ya 10% ya Halmashauri vinapewa mafunzo ya biashara ili kuongeza tija ya Mikopo hiyo.

**681. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia upya Kodi mbalimbali zinazotozwa kwenye Shule Binafsi ili kuzipa nafuu Shule hizi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**682. MHESHIMIWA TIMIDA MPOKI FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuifanya Ushirika kuwa na mtazamo wa Kitaifa ili kuhusisha Sekta zote za uzalishaji mali badala ya kilimo tu.

**683. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Bonde la Mto Baray - Karatu.

**WIZARA YA AFYA:**

**684. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambayo ni msaada mkubwa kwa Wananchi wa Musoma Mjini.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**685. MHESHIMIWA SALEHE MBWANA MHANDO (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi katika Kata za Kiberashi na Masagalu ili kuimarisha usalama wa Wananchi.

**WIZARA YA UJENZI:**

**686. MHESHIMIWA MOSES CHARLES BUJAGA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Kabila – Maligisu – Kadashi – Bukwimba km 31.73 itakamilika kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Majimbo ya Sumve na Magu.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 *(The Finance Bill, 2026)*.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**25 JUNI, 2026** **KATIBU WA BUNGE**